

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI KWA WAWEZESHAJI WANAWAKE KATIKA UENDESHAJI WA MIDAHALO YA KIJAMII KUHUSU MASUALA YA USULUHISHI NA UTATUZI WA MIGOGORO YA KIJAMII

Jumuiya ya Wanawake wenye Ulemavu Zanzibar (JUWAUZA) inatangaza nafasi 4 kwa wanawake tu, watakaoendesha midahalo kwa makundi mbalimbali katika jamii katika kutatua migogoro na kujenga maridhiano kwenye jamii zao. Shughuli zote za mradi zimefadhiliwa na Foundation for Civil Society wakishirikiana na Search for Common Grounds.

Mradi huu uitwao “Tushiriki Pamoja” utawafikia wanajamii Kupitia midahalo 8 ya kijamii, katika shehia ya Daraja Bovu (Mtopepo) na shehia ya Uzini Unguja. Midahalo hiyo itaongozwa na wanawake watakao tambulikana kama “**Community Dialogue Facilitators**” (wawezeshaji wa midahalo ya Kijamii).

MALENGO YA MRADI:

- Kuwajengea uwezo wawanawake katika ushiriki wa masuala ya maridhiano pamoja na kuwajengea uwezo wanajamii wa makundi mbalimbali katika masuala ya usuluhishi wa migogoro katika jamii
- Kutengeza jukwaa la majadiliano litakaloibuwa mapendekezo yatakayopunguza mivutano na kuimarisha mshikamano kwa jamii.

SIFA ZA MUOMBAJI:

- Awe mwanamke, Mzanzibari, Umri kati ya miaka 18-40
- Awe anajua kusoma na kuandika Kiswahili na Kiingereza kwa ufasaha.
- Awe na uzowefu wakuendesha midahalo ya kijamii usiopungua miaka 2
- Awe na uwezo wa kuandika ripoti kwa kiingereza na kukabidhi ofisini ndani ya siku tatu baada ya kukamilika kwa mafunzo au midahalo.
- Awe mchapakazi na uwezo wakufanya kazi kwa mashirikiano
- Uzoefu wa matumizi ya kompyuta.

MAJUKUMU YA KAZI

- Atafanya kazi kwa kushirikiana na Afisa muendeshaji wa mradi huu katika kupanga, kuratibu pamoja na kuendesha midahalo kwenye jamii,
- Kuendesha mazungumzo katika midahalo na Kuchukua mapendekezo ya washiriki na kuandika ripoti
- Kushirikiana na na watendaji wa mradi katika Ufatiliaji na tathmini wa shughuli za mradi.

Muda wa mradi: Mradi huu ni wa miezi sita, kuanzia **1/10/2021-30/3/2022**.

Kituo cha Kazi: Unguja

Utaratibu wa Malipo

- Wawezeshaji midahalo watakoachaguliwa watalipwa kwa kila mdahalo baada ya kukamilisha ripoti ya shughuli husika ndani ya siku tatu.

Nakala za kuambatanisha kwa Waombaji ni:

- Barua ya maombi
- Taarifa Binafsi (CV), itakayoonesha anuani na njia za mawasiliano na uzowefu kwa nafasi anayoomba na wadhamimi wasiopungua wawili.

NAMMNA YA KUWASILISHA MAOMBI:

- **Kwa njia ya Barua, Maombi yaandikwe kwa Anuani ifuatayo:**

Mkurugenzi Mtendaji

Jumuiya ya Wanawake Wenye Ulemavu Zanzibar

P.O.Box 1731

Zanzibar

- **Kwa njia ya Barua pepe:**

Barua Pepe: info@juwauza.or.tz

Wanawake wenye Ulemavu wenye sifa zinazotakiwa watapewa kiapaombele. Mwisho wa kutuma Maombi ni Tarehe **25/10/2021**, Saa za Kazi.